

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII
IDARA YA WANYAMAPORI**



Chuo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa
Maliasili kwa Jamii (CBCTC) Likuyu
Sekamaganga,
S.L.P 24,
NAMTUMBO/RUVUMA
TANZANIA.

Simu: 0252951050

Barua pepe: cbctc@maliasili.go.tz

Tovuti: www.cbctclikuyu.ac.tz

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.Na.GD/CBCTC/AD/BTCTG/....

Tarehe: 20/09/2021

Bw/Bi.....

S.L.P

.....

**KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA CHUO KWA KOZI YA ASTASHAHADA YA AWALI YA
WAONGOZA WATALII, KWA MWAKA 2021/2022**

Nakujulisha kuwa, umechaguliwa kujiunga na Chuo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii – Likuyu Sekamaganga kwa kozi ya Astashahada ya Awali ya Waongoza watalii kwa mwaka 2021/2022.

1. MAHALI CHUO KILIPO

Chuo kipo kilometa 40 kutoka Makao Makuu ya Wilaya ya Namtumbo, Mkoani Ruvuma. Kimepakana na Hifadhi ya Taifa ya Nyerere, Ushoroba wa Selous-Niassa na Hifadhi ya Jumuiya ya Mbarang'andu. Ujirani na maeneo haya ya hifadhi unakifanya chuo kiwe na mazingira mazuri na halisi kabisa kwa utoaji wa mafunzo kwa vitendo.

2. TAREHE YA KURIPOTI CHUONI

Unatakiwa kuripoti chuoni kuanzia tarehe 18 - 22/10/2021 kwa ajili ya usajili, masomo yataanza tarehe 25/10/2021.

3. MAHITAJI KWA AJILI YA USAJILI

Unatakiwa kufika na vitu vifuatavyo ili uweze kusajiliwa;

- a) Namba ya usajili uliyotumiwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi kupitia ujumbe mfupi wa simu.
- b) Vyeti halisi vya Elimu ya sekondari (Taaluma) ikiwemo ; hati ya matokeo ya mtihani (Examinations Result slip), Cheti cha kuzaliwa au kiapo cha mahakama iwapo hutakuwa na cheti cha kuzaliwa, Risiti ya benki uliyolipia ada na michango mingine na Picha ndogo (passport) nne za rangi ya bluu.

Zingatia: Udahili utakuwa batili pindi tu mhusika atakapobainika kuwa ametoa taarifa/utambulisho usio sahihi au vyeti visivyo halisi wakati wa udahili. Pia mhusika anaweza kuchukuliwa hatua za kisheria ikiwemo kushtakiwa na kufutiwa udahili. Iwapo tatizo hilo litatokea, Chuo hakitarudisha malipo yoyote ambayo yatakuwa tayari yameshafanywa.

c) **UPIMAJI WA AFYA**

- i) Kutokana na aina ya mafunzo yatolewayo ambayo ni Jeshi Usu, ili mwanafunzi aweze kusajiliwa atatakiwa kuwasilisha taarifa ya kiafya inayothibitisha kuwa yeye ana afya njema na anaweza kujiunga na mafunzo haya. Hivyo, unatakiwa kupima afya na upimaji huo ufanyike na daktari aliyesajiliwa kutoka katika hospitali za Serikali. Fomu iliyoambatanishwa itumike na daktari kwa ajili ya kujaza taarifa zako za kiafya.

Zingatia: Nakala halisi ya fomu ya taarifa za kiafya iwasilishwe Chuoni siku ya usajili, usiitume kwa njia ya posta au barua pepe.

- ii) Kila mwanafunzi anawajibika kulipia gharama za upimaji wa afya yake.
- iii) Chuo kinatoa huduma ya kwanza tu, iwapo mwanafunzi atakuwa na tatizo la kiafya litakalomlazimu kupata matibabu katika hospitali yoyote nje ya Chuo, atawajibika kulipia gharama za matibabu. Hivyo kwa mwanafunzi ambaye tayari ana kitambulisho cha bima ya afya anashauriwa kuja nacho Chuoni. Kwa ambaye hana kitambulisho hicho, anashauriwa kuja Chuoni na Tsh. 50,400/= ili afanyiwe utaratibu wa kujiunga na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na kupata kitambulisho ambacho kitatumika kwa matibabu kwa kipindi cha mwaka mmoja.

iv) **UTARATIBU WA MALIPO YA ADA**

A. GHRAMA YA MAFUNZO				
S/N	AINA YA MALIPO	MUHULA WA KWANZA (TSH)	MUHULA WA PILI (TSH)	JUMLA (TSH)
1	Ada	420,000	420,000	840,000
2	Mafunzo kwa vitendo	105,000	105,000	210,000
3	Chakula	480,000	480,000	960,000
4	Malazi	48,000	48,000	96,000
JUMLA NDOGO		1,053,000	1,053,000	2,106,000
B: MICHANGO MINGINE				
6	Ada ya usajili	10,000	0	10,000
7	Sare (Jozi moja ya Kombati , Kauda suit, buti na socks) pamoja na tisheti moja	210,000	0	210,000
8	Michezo na Burudani	5,000	0	5,000
9	Gharama ya udhibiti wa ubora wa viwango vya mafunzo (Inapokelewa na Chuo kwa niaba ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi – NACTE)	15,000	0	15,000
10	Huduma ya kwanza	10,000	0	10,000
11	Fedha ya tahadhari	10,000	0	10,000
12	Umoja wa wanafunzi	5,000	0	5,000
13	Kitambulisho	10,000	0	10,000
14	Gharama ya cheti	0	25,000	25,000
JUMLA NDOGO		275,000	25,000	300,000
JUMLA KUU (A + B)		1,328,000	1,078,000	2,406,000

Malipo yote yafanyike kupitia benki ya NMB au wakala wa NMB mahali popote nchini kwenye akaunti ya chuo yenye jina lifuatalo; CHUO CHA LIKUYU SEKAMAGANGA, namba ya akaunti 62401100011. Kutokana na sababu za kiusalama, mwanafunzi anashauriwa kutosafiri na fedha taslimu za ada au michango mingine.

ZINGATIA: Mwanafunzi hatasajiliwa kwa masomo ya muhula wowote iwapo atakuwa hajakamilisha malipo ya ada na michango mingine kama inavyooneshwa kwenye jedwali hapo juu.

4. CHAKULA NA VINYWAJI

Chakula kitatolewa na Chuo kwa sababu gharama zake tayari zimeshaingizwa kwenye ada. Vinywaji baridi pekee ndivyo vitakavyoruhusiwa kuwepo katika mazingira ya Chuo na vitapatikana kwa gharama ya mwanafunzi. Vinywaji vyenye kilevi na vingine vinavyohusiana na ulevi haviruhusiwi mahali popote Chuoni.

5. MALAZI

Malazi yanapatikana chuoni kwa sababu gharama zake tayari zimeshaingizwa kwenye ada.

6. VIFAA VYA MALAZI

Unatakiwa kuja na vifaa vifuatavyo kwa ajili ya malazi:

- i) Mashuka mawili (2) ya rangi ya bluu bahari au pinki
- ii) Taulo moja (1)
- iii) Sweta / koti zito moja (1)
- iv) Blanket zito moja (1)
- v) Koti la mvua moja (1)

NB: Magodoro yanapatikana Chuoni.

7. SARE NA NGUO ZA MICHEZO

Mwanafunzi anatakiwa kuja na sare zifuatazo;

- i) Jozi moja ya (1) " Track suit" ya rangi ya bluu bahari au nyeusi
- ii) Jozi moja (1) ya viatu nyeusi (visivyo na kisigino)
- iii) Jozi mbili (2) za socks nyeusi
- iv) Nguo za michezo (Raba, bukta na Tisheti)

8. MAFUNZO KWA VITENDO

Kutakuwa na mafunzo kwa vitendo kwa kila muhula yenye lengo la kuwafanya wanafunzi watekeleze kwa vitendo yale waliyojifunza katika muhula husika. Alama za mafunzo kwa vitendo zitajumuishwa kwenye alama za majaribio ya muhula husika. Gharama za mafunzo kwa vitendo zitatolewa na Chuo kwa sababu tayari zimeshaingizwa kwenye ada.

9. MAHITAJI BINAFSI YA MWANAFUNZI

Ni wajibu wa mzazi / mfidhili kuhakikisha mwanafunzi anapata mahitaji binafsi kwa kipindi chote cha masomo ili kumuwezesha kujifunza kwa ufanisi.

10. HUDUMA ZA PHOTOCOPY

Huduma za photocopy zinapatikana chuoni kwa gharama nafuu. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuwa na fedha za ziada kwa ajili ya huduma hizo.

11. UMOJA WA WANAFUNZI

Kuna umoja wa wanafunzi unaoitwa "Community Based Conservation Training Centre Students Organization" (CBCTCSO) ambapo, kila mwanafunzi anayesajiliwa kujiunga na Chuo anakuwa mwanachama moja kwa moja. Kila mwanafunzi anatakiwa kulipia Tsh. 5,000 kama gharama za umoja huo kama inavyooneshwa katika jedwali hapo juu.

12. SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA CHUO

Mwanafunzi lazima azingatie na kufuata sheria, kanuni na taratibu za Chuo ambazo ataelekezwa na kukabidhiwa mara tu baada ya kusajiliwa. Pia sheria, kanuni na taratibu hizi zinapatikana kwenye maktaba, kitabu cha taarifa za chuo (Prospectus) na kwenye tovuti ya Chuo. Hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa kwa mwanafunzi atakayevunja sheria, kanuni na taratibu za chuo.

13. USAFIRI

Mwanafunzi anatakiwa kufanya taratibu za usafiri wa kumfikisha Chuoni kulingana na mahali anapotoka.

14. MAWASILIANO

Kwa maelezo zaidi wasiliana na Chuo kupitia anuani ifuatayo:

MKUU WA CHUO,
CBCTC-Likuyu Sekamaganga,
P.O BOX 24,
Namtumbo, Ruvuma.
Simu Mezani: 025 295 1050,
Simu Na: 0754 352 846/0788 409 433,
Barua Pepe: cbctc@maliasili.go.tz
Tovuti: www.cbctclikuyu.ac.tz

AFISA UDAHILI,
Simu Na: 0753 478 307

"KARIBU SANA"

**MINISTRY OF NATURAL RESOURCES AND TOURISM
WILDLIFE DIVISION**



**COMMUNITY BASED CONSERVATION TRAINING CENTRE (CBCTC)
LIKUYU SEKAMAGANGA**

MEDICAL EXAMINATION FORM

NOTES:

The candidate is likely to undergo prolonged physical exertion at high temperature in remote areas. He/she must be capable of walking considerably distances and must have full use of both legs, arms and hands all fingers.

INSTRUCTIONS:

1. The medical examiner must be a dully registered Medical Practitioner
2. This form should be completed using BLOCK LETTERS.
3. This form once completed should be sealed by the Medical Examiner separately from the Application Form.

PART A: PERSONAL DETAILS (To be completed by the applicant)

1. SURNAME OR FAMILY NAME.....
2. OTHER NAMES.....
3. SEX.....
4. DATE OF BIRTH.....
5. NATIONALITY.....
6. MAILING ADRESS.....

**PART B: DECLARATION (To be completed by the applicant in presence of the
Medical Examiner)**

I declare that, to the best of my knowledge I am not suffering from any physical disability of which I have not informed the Medical Examiner and that the statements made and information given by the Medical Examiner about me is correct.

Applicants signature Date.....

PART C: MEDICAL EXAMINATION FORM (To be completed by the Medical Examiner)

1. Body Weight Height.....

2. Blood Analysis: Total WBC..... /m, LYMPHOCYTES
.....% NEUROPHYL.....%,
EUSINOPHYL.....% MONOCYTES.....%
, E.S.R.....mm/hr

3. CARDIOVASCULAR SYSTEM Pulse Rate...../Min,
Rhythm..... BP..... mm/Hg

4. RESPIRATORY SYSTEM
XRAY.....

5. ABDOMEN
Spleen.....Liver.....Kidney.....

6. NERVOUS SYSTEM Any Mental Disorder: YES / NO

7. EYES Normal: YES / NO Visual Acuity: Left Eye..... , Right
Eye.....

8. EARS Normal: YES / NO Any Discharge: YES / NO

9. URINE ANALYSIS Urine Sed, Urine Protein

10. STOOL ANALYSIS Stool for Ova: YES / NO

11. PHYSICAL DISABILITY (Given Details)
.....

12. RECOMMENDATIONS
.....
.....
.....

- NAME.....
SIGNATURE.....
DESIGNATION.....

- OFFICIAL STAMP.....
DATE.....